

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



**MAELEZO YA NAIBU SPIKA
KUHUSU UGAWAJI WA
MADAWATI**

Mheshimiwa Rais;

Waheshimiwa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge;

Waheshimiwa Mawaziri;

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;

Waheshimiwa Wabunge;

Mheshimiwa Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam;

Waheshimiwa Wastahiki Meya wa Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam;

Wakuu wa vyombo vyta Ulinzi na Usalama;

Viongozi Waalikwa;

Mabibi na Mabwana.

- 1.0 Kwa niaba ya Mhe. Spika na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Bunge, natumia fursa hii kukukaribisha na kukushukuru kwa dhati kwa kukubali kwako kuwa Mgeni Rasmi katika hafla hii fupi ya uzinduzi wa mpango wa ugawaji wa madawati.
- 2.0 Mnamo tarehe 11 Aprili, 2016 wakati wa hafla fupi iliyofanyika IKULU, Dar es Salaam, Ofisi ya Bunge ilikukabidhi kiasi cha Shilingi Bilioni Sita kwa ajili ya kutengeneza madawati. Fedha hizo zilitokana na mpango wa Serikali wa kubana matumizi. Katika kutekeleza agizo hilo, Ofisi ya Bunge ilitoa kiasi hicho kutoka kwenye Mfuko wa Bunge (*The National Assembly Fund*) ikiwa ni mchango

wa Wabunge katika jitihada za Serikali za kuhakikisha madawati ya kutosha yanapatikana kwenye Shule za Msingi hapa Nchini. Kazi hiyo ya utengenezaji wa madawati imetekelizwa na Jeshi la Magereza na SUMA JKT kwa makubaliano kuwa ikamilishwe kwa awamu mbili.

- 3.0 **Mhe. Rais**, kazi hii ilitarajiwa kukamilika kwa awamu ya kwanza tarehe 15 Julai, 2016. Hata hivyo, kutokana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake, kazi hiyo haikukamilika kwa wakati uliopangwa. Aidha, kumekuwa na juhudzi zinazofanywa na Jeshi la Magereza na SUMA JKT kukamilisha awamu ya kwanza ifikapo tarehe 30 Julai, 2016 na awamu ya pili tarehe 30 Septemba, 2016.

- 4.0 **Mhe. Rais**, naomba kukuarifu kuwa, kazi ya utengenezaji wa madawati yapatayo elfu sitini katika awamu ya kwanza tayari imekamilika kwa kiwango kikubwa na tumearifiwa kuwa jumla ya madawati **53,450** yamekamilika. Tume ya Utumishi wa Bunge imeandaa utaratibu na vigezo vya ugawaji wa madawati hayo. Vilevile, Tume imeandaa idadi ya mgao wa madawati katika Mikoa itakayopata katika Awamu ya Kwanza na Mikoa itakayopata katika awamu ya pili.
Vigezo vilivyozingatiwa na Tume ya Utumishi wa Bunge ni pamoja na:-

- (i) Uwiano wa pande zote Mbili za Muungano, yaani, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na

(ii) Utayari wa madawati ya kutosheleza katika kanda mbili. Kanda hizo ni:- Kanda ya Mashariki na Pwani na Kanda ya Nyanda za Juu na Kusini.

5.0 **Mhe. Rais**, Mikoa itakayohusika kwenye awamu ya kwanza ya ugawaji madawati ni ifuatayo:-

1. Pwani, 2. Morogoro, 3. Mtwara, 4. Lindi, 5. Ruvuma, 6. Iringa, 7. Njombe, 8. Mbeya 9. Songwe, 10. Rukwa, 11. Katavi, 12. Visiwa vya Unguja, 13. Pemba 14. Tanga na 15. Mkoa wa Dar es Salaam ambao nitakuomba hivi punde uweze kukabidhi jumla ya Madawati **537** kwa Mhe. Mussa Azzan Zungu Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi la Ilala kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote wenye majimbo ya uchaguzi hapa nchini.

Utaratibu wa ugawaji wa madawati haya kwenye Mikoa hiyo unatokana na ukaribu wa maeneo hayo na maeneo yalipotengenezwa madawati. Maeneo ya viwanda hivyo ni:-

- i. Ukonga - Magereza
- ii. JKT - Chang'ombe
- iii. Itende - Mbeya
- iv. Mafinga – Iringa
- v. Mlale – Songea na
- vi. Maramba – Tanga

Na hivyo kupunguza gharama za kusafirisha madawati kwa umbali mrefu.

- 6.0 **Mhe. Rais**, katika awamu hii ya kwanza tunatarajia kugawanya jumla ya madawati **61,385**, utakao husisha jumla ya Majimbo ya Uchaguzi **155** kati ya Majimbo **264**. Kiuwiano wa majimbo ni sawa na Asilimia **59** wa madawati yote **120,000**. Aidha, ugawaji wa madawati katika awamu ya pili ambayo JKT na Magereza wametuthibitishia yatakuwa tayari ifikapo tarehe 30 Septemba, 2016, utahusisha kanda zingine mbili za mikoa ya kanda ya Kaskazini na Ziwa na Kanda ya Kati na Magharibi.
- 7.0 **Mhe. Rais**, napenda kukuarifu kuwa tayari tumekubaliana na Jeshi la Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuwa madawati ya awamu ya pili yatatengenezwa kwenye viwanda vingine vilivyo kwenye Kanda hizo. Viwanda hivyo ni vifuatavyo:-

- i) JKT Kanembwa na Mtabila Mkoani Kigoma
- ii) Uyui -Tabora
- iii) Samani -Arusha na
- iv) Kiwira – Mbeya

Utaratibu huu utasaidia kwa kiasi kikubwa, kupunguza ghamama za usafiri, kuepusha uharibifu, na kuhakikisha ubora wa madawati hayo.

8.0 **Mhe. Rais**, baada ya maelezo hayo naomba nichukue fursa hii kukukaribisha rasmi ili uweze kufanya uzinduzi wa mpango wa ugawaji wa madawati laki moja na ishirini yatakayogawiwa kwa awamu mbili; Awamu ya kwanza ya madawati elfu sitini ikianza leo.

Mhe. Rais, Karibu sana.

Dkt. Tulia Ackson (Mb)

NAIBU SPIKA

13 Julai, 2016